



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA



**TANGAZO LA KUKODISHA SHAMBA LA BULYASHIRI LINALOMILIKIWA NA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA**

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga anawatangazia wananchi wote kwamba, Halmashauri inakodisha shamba la Bulyashiri lipo katika kata ya Nguvumoja kijiji cha Mwalala lenye ukubwa wa ekari 652 kwaajili ya shughuli za kilimo katika msimu wa mwaka 2022/2023.
2. Hivyo, mazao yanayoruhusiwa kulimwa ni yale ya muda mfupi kama vile karanga, mahindi, alizeti, njugumawe, mtama, kunde, maharage na viazi vitamu.
3. Mwananchi atakaependa kukodi shamba atatakiwa kulipa gharama ya TZS 30,000/= (Elfu thelathini tu) kwa kila ekari moja kwa msimu mmoja tu. Fedha hizi zitalipwa kupitia akaunti ya Halmashauri baada ya kupewa barua ya tuzo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga na kusaini mkataba.


MAMBO YA KUZINGATIA:

1. Mwombaji atatakiwa kuandika barua ya kuomba kulima ikianisha mazao atakayolima na ukubwa wa eneo analohitaji.
2. Barua ya mwombaji ionyeshe jina la mwombaji, mahali anapoishi, namba ya simu, namba ya kitambulisho cha Taifa au kitambulisho cha mpiga kura.
3. Maombi yawasilishwe kwa mkono kwenye ofisi ya Kitengo cha Manunuzi, Halmashauri ya Wilaya ya Igunga katika bahasha iliyofungwa vizuri, juu ya bahasha yaandikwe maneno yafuatayo:

“OMBI YA KUKODISHA ENEO KATIKA SHAMBA LA BULYASHIRI”

4. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **17 Octoba 2022 saa 5.00 (tano) kamili asubuhi**. Maombi yatakayochelewa hayatafanyiwa kazi. Wananchi wote watakaoleta maombi watapewa majibu.

Limetolewa tarehe 03 Oktoba 2022 na:


JOSEPH E. SAMBO
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
IGUNGA
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

Halmashauri ya Wilaya, S.L.P 19, Igunga. Simu: +255 (026)-2650019, +255 (026) 2650021.
Nukushi +255 (026) 2650242. Barua pepe: ded@igungadc.go.tz. Tovuti: <http://www.igungadc.go.tz>